Namba ya mtahiniwa.....

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SEREKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA KILOMBERO

MTIHANI WA UTAMIRIFU KWA KIDATO CHA PILI

021 **KISWAHILI**

MUDA: **Masaa 2.30** Alhamisi, 03 Septemba 2019

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Majibu **yote** yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa.
4. Majibu **yote** yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
5. Vifaa **vyote** vya mawasiliano **haviruhusiw**i katika chumba cha mtihani.
6. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
NAMABA YA SWALI	**ALAMA**	**SAINI YA MTAHINI**
1		
2		
3		
4		
5		
JUMLA		

SEHEMU A (Alama 15)
UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.
Ilikuwa siku ya Jumamosi wakati watu wengi hawaendi kazini, siku hiyo watu wengi huwa kwenye michezo, wengine kwenye vilabu vya pombe na wengine huenda **gulioni**. Hapo ndipo palipokuwepo na mnada **kabambe**.

Umati wa watu ulikuwa umezunguka uzio ambao ulikuwa ni wa kamba ya katani, ambao ndani yake alikuwepo bwana mmoja mrefu mweusi tii, mwenye shingo ndefu kama twiga, alivaa kanzu nyekundu na kofia ya tarabushi. Huyo ndiye aliyekuwa dalali wa siku hityo, alishika beberu lililopea ambalo ndevu zake ziligusa ardhini.

Dalali alianza kulinadi beberu kwa kusema “Haya leo tena jamani sogeeni mmjipatie vitu vya bei poa, oneni mnyama mnono huyu”. Alimgeuza kila upande ili watu wapate kumuona. Kisha aliendelea kumnadi “ Anauzwa kwa **buku** sita tu, nani amtakaye na atanipa ngapi?” Mteja mmoja alipandisha bei akasema “ Ninaongeza shilingi elfu kumi” mteja mwingine akasema “Naongeza elfu nne ziwe elfu ishirini”

Dalali akaligeuza tena beberu kwa hadhira huku akisema ‘” **Mnalideku** hili beberu? Ona lilivyonona”. Toka hapo bei ikazidi kupanda ajabu, hatimaye akajitokeza babu aliyekuwa amevaa kanzu na kizibao, kichwani ametinga kilemba, kwa sauti akikoloma akasema “Mimi naongeza buku kumi”. Dalali akasema “Buku thelathini kwa mara ya kwanza, buku thelethini kwa mara ya pili, buku thelathini kwa mara ya tatu” Hakuna mtu aliyejitokeza kupandisha dau. Dalali akamwambia babu “Haya lipa hela chukua baberu lako”. Babu akalipa elfu thelathini akachukua beberu akaendanae nyumbani kwake.

Maswali

a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano. _____

b) Eleza wasifu wa dalali
i) _____
ii) _____
iii)_____

c) Kitu gani kinachoonesha kuwa beberu lilikuwa limepea?
_____

d) Kwa sababu gani wateja walikuwa wanaongeza bei?

_____

e) Eleza kwa ufupi maana za manen yafuatayo kama yalivyotumika kwenye habari

i) Gulioni _____

ii) Mnalideku _____

iii) Buku_____

iv) Kabambe _____

f) Fupisha habari uliyosoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi themanini (80).

SEHEMU B (Alama 15)
UTUMIZI WA LUGHA NA USAHIHI WA MAANDISHI

2. a) Andika kwa usahihi maneno yaliyokolezwa wino kama yalivyotumika katika tungo zifuatazo;

i) Hakuna mtu **yoyote** aliyefika. _____

ii) Viongozi **wamewakilisha** michangoyote. _____

iii) Baada ya mahojiano, **mwisho wa siku** mambo yalikuwa sawa.

_____

iv) Kila siku **naendaga** shule. _____

v) Baba ameuza mbuzi **zake** wate. _____

b) Kwa kila kauli hapo chini, andika KWELI kwa kauli ambayoni sahihi na SI KWELIkwakauli ambayo si sahihi mbele yake.

i) Msimu rejeshi ni aina ya msimu ambao huenea karibu nchi nzima

_____

ii) Sarufi maumbo ni taaluma inayoshughulikia matamshi sahihi ya maneno katika lugha husika _____

iii) Kufupisha maneno ni njia mojawapo ya kuunda msimu _____

iv) Rejesta ni mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira maalum

_____

v) Fasihi ni kazi ya lugha ambayo si ya kisanaa_____

c) Panga maneno yafuatayo kama yanavyotakiwa kuwa katika kamusi.

a) Zawadi	a)_____
b) Sherehe	b)_____
c) Bugudha	c)_____
d) Brigadia	d)_____
e) Chakula	e)_____
f) Alfajiri	f)_____
g) Jahazi	g)_____
h) Nakshi	h)_____
i) Muktadha	i)_____
j) Darubini	j)_____

SEHEMU C (Alama 20)
SARUFI

3. a) Nyambulisha maneno yafuatayo kwa kuunda maneno mawili kwa kila neno

i) Cheza _____
ii) Pata _____
iii) Sema _____
iv) Piga _____
v) Acha _____

b) Bainisha vitenzi vishirikishi katika sentensi zifuatazo

i) Huyu si mtu mwema _____
ii) John alikuwa mwizi sana _____
iii) Mungu yu mwema_____
iv) Baba yetu ni mpole sana _____
v) Shaibu hakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu_____

c) Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo

i) ulinzi _____
ii) Tungo _____
iii) Mchezo _____
iv) Sifa _____
v) Tendo _____

d) Tunga sentensi kwa kutumia aina za maneno zifuatazo;

Mfano; (‘**Mimi’** litumike kama kiwakilishi)

Mimi nitacheza mpira

i) **‘Lile’** litumike kama kivumishi

_____

ii)’ **Ni’** litumike kama kitenzi kishirikishi

_____

iii) ‘**Lo!!’** Litumike kama kihisishi

_____

iv) ‘**Alikuwa’** litumike kama kitenzi kisaidizi

_____

v) ‘**Ugonjw**a’ litumike kama nomino

_____

SEHEMU D (Alama 40)
FASIHI SIMULIZI

4. a) Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata

1. Moyo nimeushauri, lakini umekaidi
Moyo kiburi hatari, mfano wa kama radi
Moyo mefumbata shari, ulonayo makusudi
Moyo u mwilini mwangu, jirudi tuwe pamoja.

2. Unaona yasofaa, yaache hayo matata
Hata kama vyang'aa, mbali navyo wewe pita
Huu ndio ushujaa, na kwa hayo hutojuta
Moyo usongeze dundo, taratibu ndio mwendo

3. Moyo jifunze busara, iwe ndio yako taa
Usilinge na ukora, mivuto hiyo kataa
Chunguza zile ishara, zenye kuleta tamaa
Zikariri moja moja, zikipita zikwambie

4. Moyo madhira kataa, nipate kwako tulia
Mengi nimeyajulia, mabaya kuyatambua
Nisije kuangamia, tama zikinijia
Naomba moyo tulia, nipate yakobusara

5. Moyo punguza ubaya, nipate yako mazuri
Baadae sije kupwaya, nikakosa yako kheri
Kwangu hakuna ubaya, kwako wewe nashari
Moyo punguza hasira, nipate zako fadhira.

Maswali

i) Bainisha muundo na mtindo wa shairi hili;
Muundo wa shairi ni _____
Mtindo wa shairi ni _____

ii) Eleza dhamira ya mtunzi katika ubeti wa tau
_____

iii) Eleza ujumbe wa shairi hili
_____

iv) Bainisha vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa pili
_____

v) Andika kichwa cha habari kisichozidi maneno matano
_____

b) Tegua vitendawili vifuatavyo

i) Nyuma yangu ina nguzo moja _____

ii) Nasuka mkeka lakini ninalala chini _____

iii) Nikipiga mwana ngu watu hucheza _____

iv) Anatembea na nyumba yake _____

v) Upala wa babu unafuka moshi _____

c) Eleza kwa ufupi maana ya dhana zifuatazo

i) Kisasili

_____

_____

ii) Ngonjera

_____

_____

iii) Fasihi

_____

_____

iv) Tarihi

_____

_____

v) Nyimbo

_____

_____

d) Chagua neno sahihi kutoka kwenye kisanduku ili kukamilisha maana kutoka katika sentensi ulizopewa.

Sanaa, methali, nahau, ngano, soga, semi, kejeli

i) Ni hadithi fupi ambazo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, hutolewa ili kutoa maadili _____

ii) Tanzu zake ni methali, vitendawili,misemo, na mafumbo

_____

iii) Ufundi wa kuwasilisha mawazo yaliyo katika fikra za binadamu

_____

iv) Ni hadithi fupi za kukejeli na kuchekesha _____

v) Kimuundo zina uwili na mpangilio wenye ukinzani _____

SEHEMU E (Alama 10)
UANDISHI WA INSHA/ UTUNGAJI

5. Andika barua ya kuomba kazi ya ukarani kwenye kiwanda cha sukari Kilombero, barua ielekeze kwa meneja uajili. Jina lako liwe Patrick Sibomana S. L. P 14

Mlandizi.

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALIMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO
MUONGOZO WA USAHIHISHAJI MTIHANI WA UTIMILIFU WILAYA KIDATO CHA PILI
KISWAHILI

SEHEMU A (Alama 15)
UFAHAMU

1. a) MNADA WA BEBERU **Alama 01**

   b) i) Mwusi
   ii) Shingo ndefu **Alama 03 @ 01**
   iii) Mrefu

   c) Beberu lilikuwa limenona **Alama 01**

   d) Kwa sababu beberu alikuwa mkubwa **Alama 01**

   e) i) Soko/ mnada
   ii) Mnaliona? **Alama 04 @ 01**
   iii) Elfu moja
   iv) Mkubwa/unaovutia/ unaosisimua

   f) Mambo ya kuzingatia **Alama 05**
   - Afuate taratibu zote za uandishi
   - Abainishe mawazo makuu katika aya na kuhusisha na habari
   - Azingztie idadi ya maneno

SEHEMU B (Alama 15)
UTUMIZI WA LUGHA NA USAHIHI WA MAANDISHI

2. a) i) Yeyote
   ii) Wamewasilisha
   iii) Hatimaye **Alama 05 @ 01**
   iv) Huwanaenda
   v) Wake

   b) i) SI KWELI
   ii) SI KWELI
   iii) KWELI **Alama 05 @ 01**
   iv)KWELI
   v) SI KWELI

   c) a) Alfajiri
   b) Brigadia
   c) Bugudha

d) Chakula
e) Darubini
f) Jahazi **Alama 05 @ 0.5**
g) Muktadha
h) Nakshi
i) Sherehe
j) Zawadi

SEHEMU C (Alama 20)
SARUFI

3. a) i) Chezesha, chezeka
ii) Patana, patanisha
iii) Semea, semwa
iv) Pigwa, pigiana **Alama 05 @ 01**
v) Achana, achiana

b) i) Si
ii) Alikuwa
iii) Yu **Alama 05 @ 01**
iv) Ni
v) Hakuwa

c) i) Linda
ii) Tunga
iii) Cheza **Alama 05 @ 01**
iv) Sifu
v) Tenda

d) i) Gari **lile** ni zuri sana
ii) Huyu **ni** mwema
iii) **Lo!!** Wamefariki wote **Alama 05 @ 01**
iv) Mtoto **alikuwa** anacheza mpira
v) **Ugonjw**a huu umeenea sana

SEHEMU D (Alama 40)
FASIHI SIMULIZI

4. a) i) Muundo wa shairi ni TARBIA (Mishororo minne)
Mtindo wa shairi ni wa KIMAPOKEO
ii) Umuhimu wa kutumia busara

iii) Tuache tamaa **Alama 05 @ 01**
iv) Kati “a” na mwisho “ta”
v) MOYO USIWE NA TAMAA

b) i) Uyoga
ii) Boga
iii) Ngoma **Alama 05 @ 01**
iv) Kobe
v) Ugali wa moto

c) i) Ni hadithi fupi zinazoelezea asili ya mambo mbalimbali kama vile, maumbile ya watu, wanyama, asili ya kifo, mahali,tabia n.k
ii) Ni tungo zenye muundo wa mashairi ya kimapokeo na ndani yake kuna majibizano/ mazungumzo baina ya watu wawili na kuendelea.
iii) Ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. **Alama 05 @ 01**
iv) Ni hadithi fupi zinazosimulia kuhusu matukio ya kihistoria.
v) Ni mpangilio maalum wa maneno na mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti.

d) i) Ngano
ii) Semi
iii) Sanaa **Alama 05 @ 01**
iv)Soga
v) Methali

SEHEMU E (Alama 10)
UANDISHI WA INSHA/ UTUNGAJI

5. Mambo ya kuzingatia;
   - Anuani ya mwandishi **Alama 01**
   - Tarehe **Alama 01**
   - Anuani ya mwandikiwa **Alama 01**
   - Kichwa cha barua **Alama 01**
   - Kiini cha barua **Alama 02**
   - Mwisho wa barua **Alama 01**
   - Saini ya mwandishi **Alama 01**
   - Jina la mwandishi **Alama 01**
   - Uzingztiaji wa alama sahihi za uandishi **Alama 01**